

IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

Maeneo ya uwekezaji upande wa Idara ya Mifugo na Uvuvi.

- Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji na uanzishaji wa ranchi ndogo ndogo kwa ng'ombe wa nyama
- Uanzishaji wa viwanda vya maziwa na nyama
- Machinjio ya Kisasa iliyopo katika eneo la Utengule
- Fursa za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kutokana na hali ya hewa kuruhusu ufugaji wa ng'ombe wa kisasa
- Uanzishaji wa mashamba ya kutotolesha vifaranga vya kuku (Hatchery Units)
- Utoaji wa huduma za mifugo kama majosho, machinjio n.k
- Fursa za uanzishaji wa mabwawa ya samaki
- Uanzishaji wa masoko ya biashara ya samaki

SHUGHULI ZINAZOSIMAMIWA NA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

1. KITENGO CHA MIFUGO

- Ufugaji wa ng'ombe wa Nyama
- Ufugaji wa ng'ombe wa Maziwa
- Ufugaji wa Nguruwe
- Ufugaji wa Kuku asili
- Ufugaji wa Kuku wa kisasa (Nyama na Mayai)
- Ufugaji wa Mbuzi asili/kisasa
- Ufugaji wa Kondoo
- Ufugaji wa Punda
- Ufugaji wa Wanyama wengine
- Usimamizi wa huduma za Wanyama pori
- Ushauri juu ya Ufugaji bora
- Ushauri juu ya Ujenzi wa mabanda ya mifugo
- Usimamizi wa Minada na machinjio za Halmashauri na binafsi
- Ukusanyaji wa maduhuli ya serikali
- Usimamizi na Utoaji wa huduma za afya ya mifugo
- Usimamizi na Uendelezaji wa nyanda za malisho
- Usimamizi wa Sheria zinazohusu Sekta ya Mifugo

2. KITENGO CHA UVUVI

- Usimamizi wa Doria za kudhibiti biashara haramu ya samaki
- Usimamizi wa ujenzi wa mabwawa ya samaki
- Usimamizi wa vikundi vya Ufugaji wa samaki
- Usimamizi wa mabwawa ya kuzalishia vifaranga vya samaki
- Ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kutokana na sekta ya Uvuvi
- Utoaji wa elimu juu ya ufugaji bora wa samaki
- Utoaji wa elimu juu ya uvuvi bora
- Usimamizi wa Sheria za Uvuvi

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

MDC-VET Consult

Kutambulisha Huduma za Ushauri Mifugo

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kupitia kitengo cha **Huduma za Ushauri na Tiba ya Mifugo (MDC-VET Consult)** kina wataalam wa kutosha na wenye uzoefu wa hali juu kutoa ushauri na Tiba mbalimbali juu ya huduma za mifugo kwa watu binafsi, Taasisi za Kiserikali, Mashirika ya umma, Serikali, Asasi za kiraia n.k

1. Utangulizi

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kupitia **MDC-VET Consult** huwezesha utoaji wa huduma za ushauri juu ya utoaji wa huduma za tiba ya mifugo, afya ya jamii, machinjio, mabucha, viwanda vya mazao ya mifugo, viwanda vya nyama, ubora wa madawa ya tiba ya mifugo, madawa ya kuogeshea mifugo n.k. Pia hutoa ushauri na huduma za teknolojia mbalimbali kama Uhimilishaji (AI), Upasuaji n.k.

2. Maeneo mbalimbali tunayofanyia kazi ni;

- Uchunguzi na ufuatiliaji wa magonjwa mbalimbali ya mifugo
- Uendelezaji wa nyanda za malisho
- Utoaji wa huduma za tiba, kinga na upasuaji mdogo kwa wanyama
- Uanzishaji wa miradi ya Ufugaji (Establishment of Livestock Enterprises)
- Utoaji wa huduma za afya ya jamii. (Public health services through quality control of food)
- Kiungo kati ya Serikali na Sekta binafsi
- Utoaji wa huduma za ushauri juu ya ujenzi wa mabanda ya mifugo, machinjio, majosho, minada ya mifugo, mashamba ya mifugo, mabucha na viwanda vya nyama
- Utoaji wa huduma na utunzaji na ufugaji wa mifugo juu ya upimaji wa mimba, uhimilishaji n.k
- Upasuaji na uchunguzi wa magonjwa
- Utoaji wa ushauri juu ya huduma za kisheria kwenye masuala ya afya ya jamii, machinjio, mabucha, maduka ya madawa ya mifugo, vituo vya kuendeshea huduma za mifugo, madawa ya joshu n.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na;

Dr. Samora Mshang'a (BVM)
MDC-VET Consult Coordinator,
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya
P. O. Box 253,
Mbeya, Tanzania.
Mobile: +255 767 677 615

E-mail: dr.samoraone1@yahoo.com